Name
Address Line 1
Address Line 2
Address Line 3
Address Line 4
Address Line 5

Person ID: xxxxxx Application ID: IPPA xxxxxx

**Mipango ya mpito ya kuanzishwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015**

Dear XXXXX,

Ninarejelea maombi yako ya sasa ya Hadhi ya Ukimbizi/Hifadhi Mbadala Nchini.

Ningependa kukufahamisha kwamba mipango mipya ya uchunguzi na ubainishaji wa maombi ya ulinzi wa kimataifa (hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala) na kibali cha kubakia Nchini ilianzishwa katika Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya 2015 (Sheria ya 2015) ambayo ilianzishwa na Waziri wa Haki na Usawa **mnamo tarehe 31 Desemba 2016** (“tarehe ya kuanza”).

Chini ya Sheria ya 2015, utaratibu mmoja umeanzishwa. Chini ya utaratibu huu, mwombaji ataomba Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa na Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala. Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ("IPO") itachukua nafasi ya Ofisi ya Kamishna wa Maombi ya Ukimbizi (ORAC) ambayo imeondolewa.

Mahali ambapo maombi mapya ya ulinzi wa kimataifa yamewasilishwa chini ya Sheria ya 2015, IPO itachunguza kwa wakati mmoja kama mwombaji anastahili kupewa hadhi ya ukimbizi au hifadhi mbadala au la. Kama pendelezo linalopinga litatolewa kuhusiana na hadhi hizi, Waziri ataamua, bila hatua au mawasiliano ya kiutaratibu, kama mwombaji anastahili kupewa kibali cha kusalia Nchini au la kwa sababu nyingine yoyote (ikiwa ni pamoja na masuala ya ufadhili au kibinafsi). Ruhusa ya pekee ya mchakato huu ni wakati maombi yanashughulikiwa chini ya Kanuni za EU Dublin, ambapo mipangilio mbadala

yanatumika - angalia sehemu ya 10 ya Kijitabu kilichoambatishwa cha Maelezo kwa Waomba Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1). Haya ni mabadiliko kutoka kwa utaratibu wa zamani, ambapo, kama Waziri atakunyima hadhi ya ukimbizi, Waziri angempatia mwombaji nafasi ya kuomba hifadhi mbadala na kuwasilisha kesi yake ya kwanini asipewe amri ya kufukuzwa nchini.

**HADHI YA MAOMBI YAKO**

Sheria ya 2015 ina matoleo ya mpito yanayohusiana na maombi ya hadhi ya ukimbizi na hifadhi mbadala yaliyowasilishwa kwa ORAC kabla ya kuanza kwa Sheria hiyo. Chini ya sheria ya 2015, maombi haya yatahamishwa hadi kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa ili kuchakatwa chini ya Sheria hiyo.

Maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yanashughulikiwa na **Kategoria ya 2 (Maombi ya rufaa ya ukimbizi)** katika sehemu ya 4 ya Muhtasari ulioambatishwa wa maelezo (IPO 12) kwa jina mwombaji ambaye alituma maombi ya hadhi ya ukimbizi ambayo yalikatiwa rufaa mbele ya RAT kabla ya tarehe ya kuanza lakini bado hayajaamuliwa na RAT kabla ya tarehe hiyo na, kwa hiyo, anachukuliwa kuwa ameomba ulinzi wa kimataifa chini ya Sheria ya 2015. Faili yako imehamishwa kwa IPO ili kuzingatiwa kama kuna uwezekano wa haki ya hifadhi mbadala pekee. Pendekezo la maombi ya hadhi yako ya ukimbizi lililofanywa na ORAC litahifadhiwa na litaendelea kutumika. Kama IPO itapendekeza kuwa haustahili kupewa hifadhi mbadala, basi Waziri ataamua kama unastahili kupewa kibali cha kusalia nchini. Kama utakata rufaa ya kunyimwa hadhi ya ukimbizi (iliyotolewa tayari) na hifadhi mbadala kwa IPAT, maombi hayo mawili ya rufaa yatashughulikiwa kama ombi moja na kusikilizwa kwa pamoja.

**Kwa kuwa maombi yako yaliyopo sasa ya hadhi ya ukimbizi na/au hifadhi mbadala yatazingatiwa chini ya matoleo ya mpito katika Sheria ya 2015, HUHITAJI KUTUMA MAOMBI MENGINE YA ULINZI WA KIMATAIFA. Hata hivyo, unahitajika kutoa maelezo ya ziada kwa Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa kwa kukamilisha sehemu husika za Maombi yaliyoambatishwa ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2).**

**MUHTASARI WA MAELEZO NA HATI NYINGINE ZILIZOAMBATISHWA**

Maelezo zaidi kuhusu athari ya matoleo ya mpito ya Sheria ya 2015 yameelezwa katika hati inayoitwa **"Muhtasari wa Maelezo - Mipango ya Mpito (IPO 12)."** Barua hii inastahili kusomwa pamoja na Muhtasari wa Maelezo.

Hati zifuatazo zimeambatishwa:

- **Muhtasari wa Maelezo - Mipango ya Mpito (IPO 12).**
- **Kijitabu cha Maelezo kwa Waombaji wa Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1)**, iy

- **Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa(IPO 2).**

**JE, NI SEHEMU GANI ZA DODOSO YA ULINZI WA KIMATAIFA INASTAHILI KUKAMILISHWA NA WEWE?**
Mwongozo ufuataao umetolewa kuhusu jinsi ya kukamilisha Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2).

**Unastahili kukamilisha sehemu zote za Maombi yaliyoambatishwa ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2) isipokuwa sehemu inayohusiana na hadhi ya ukimbizi (Maswali ya 63a na 63b).**

Iwapo IPO itapendekeza kuwa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yakataliwe, uamuzi utafanywa wa kama unastahili kupewa kibali cha kusalia Nchini kwa sababu nyingine au la.

Ni muhimu kukumbuka kuwa kwa kuanzishwa kwa Sheria ya 2015, utaratibu huu umebadilika. Waziri hatakuandikia tena barua akikualika uwasilishe kesi yako ya kwa nini unastahili kuruhusiwa kusalia Nchini. Badala yake, kibali cha kusalia kitazingatiwa mara moja kama IPO itapendekeza kuwa maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yanastahili kukataliwa.

Kwa hivyo, ni juu yako uelezee sababu zozote kwa kuandika barua za kwanini unaonelea unastahili kupewa kibali cha kusalia wakati unakamilisha sehemu inayofaa ya Maombi yaliyoambatishwa ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2). Kwa mfano, hali zako za kifamilia na kinyumbani, hali ya uhusiano wako na Serikali, tabia na maadili yako ndani na nje ya Nchi na sababu za kiufadhili ambazo zote ni masuala muhimu katika muktadha huu. Kwa ufafanuzi kamili wa masuala muhimu, tafadhali angalia Kijitabu cha Maelezo cha Waomba Ulinzi wa Kimataifa (IPO 1).

Unastahili pia kufahamisha IPO (kwa niaba ya Waziri) kuhusu mabadiliko yoyote ambayo yanaweza kuwa muhimu katika hali zako (k.m. hali zako za kifamilia au kinyumbani au hali kati nchi yako ya asili).

**JE, NINASTAHILI KUFANYA NINI?**
**Ukikamilisha na kutia saini Maombi ya Dodoso ya Ulinzi wa Kimataifa (IPO 2), unastahili kuyaresha kwetu, pamoja na maelezo yoyote ya ziada na hati ambazo ungependa zizingatiwe ambazo tayari hujatoa kwa ORAC, katika bahasha iliyoambatishwa ya FREEPOST. Dodoso inastahili kurejeshwa kwetu, ikiwezekana isipitishe siku 20 za kufanya kazi kuanzia tarehe ya barua hii.**

**Ikiwa wewe na/au mshauri wako wa kisheria mnahitaji kutoa maelezo ya ziada kwa IPO baada ya kuwasilisha maelezo katika aya ya 7.3 hapa juu, unastahili kufanya hivyo haraka iwezekanavyo na, kama unaweza kufanya hivyo, usipitishe wiki mbili**

**kabla ya tarehe ya mahojiano yako yaliyopangwa. Muda huu utawezesha tafsiri ya hati kama itahitajika na kuhakikisha kuwa mhojaji wa IPO ana karatasi zote zinazopatikana na kuzingatiwa mapema kabla ya tarehe ya mahojiano.**

**MAHOJIANO**
Kufuatia kupokewa kwa dodoso yako iliyokamilishwa, IPO itawasiliana na wewe kwa wakati unaofaa na tarehe ya mahojiano yako ya ulinzi wa kimataifa. Kwa kuwa tayari umepokea uamuzi kuhusu maombi yako ya hadhi ya ukimbizi, mahojiano yatashughulikia masuala ya hifadhi mbadala tu. Huenda mahojiano yako yasipangwe kwa miezi kadhaa kwa sababu ya idadi kubwa ya maombi ya kuchakatwa na IPO.

**KUISHI NCHINI**
Hali zinazohusiana na makazi yako Nchini hazitabadilika. Cheti cha Makazi ya Muda (TRC) ambacho tayari umepewa kitachukuliwa kuwa cheti cha makazi ya muda kilichotolewa chini ya Sehemu ya 17 ya Sheria ya 2015 na kitabakia halali na kinachoweza kubadilishwa hadi maombi yako ya ulinzi wa kimataifa yaamuliwe.

**USHAURI WA KISHERIA**
Unapendekezwa utafute ushauri wa kisheria kuhusiana na barua hii na hati zilizoambatishwa.
Una haki ya kushauriana na wakili na unaweza kupata huduma za Bodi ya Usaidizi wa Kisheria. Bodi ya Usaidizi wa Kisheria (LAB) ni shirika huru ambalo linatoa huduma ya kisheria ya siri kwa watu wanaoomba ulinzi wa kimataifa nchini Ayalandi. LAB itakupa usaidizi na ushauri wa kisheria wa kuunga mkono maombi yako. **Maelezo ya mawasiliano ya LAB yako kwenye Muhtasari ulioambatishwa wa Maelezo (IPO 12).**

Pia unaweza kutafuta huduma za wakili wa kibinafsi kwa gharama zako mwenyewe.

Ikiwa tayari umefanya hivyo, lazima utoe maelezo ya wakili wako wa kisheria, na ikiwezekana, mabadiliko yoyote ya wakili wa kisheria kwa Ofisi ya Ulinzi ya Kimataifa kwa haraka iwezekanavyo.

**UNHCR**
Pia una haki ya kushauriana na United Balozi Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi ambao **maelezo yao ya mawasiliano yako kwenye Muhtasari ulioambatishwa wa Maelezo (IPO 12).**

**KUREJEA KWA HIARI**
Ikiwa hutaki kuendelea na maombi yako ya ulinzi wa kimataifa, una uhuru wa kupata nafasi ya kurejea kwa hiari kwa nchi yako ya asili. Ushauri na usaidizi wa suala hili unapatikana kutoka kwa Shirika la Uhamiaji wa Kimataifa (IOM) ambao **maelezo yao ya mawasiliano yako kwenye Muhtasari ulioambatishwa wa Maelezo (IPO 12).**

**NAMBARI YAKO MPYA YA MAOMBI**
Nambari yako ya zamani ya maombi haitatumika tena. Utapata nambari yako mpya ya maombi inayoanza na **IPPA** upande wa juu wa barua hii. Kitambulisho chako cha Kibinafsi kitabakia vile vile.

**ANWANI YAKO**
Ukibadilisha anwani yako, lazima ufahamishe Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa **kwa kuandika barua** haraka iwezekanavyo baada ya kuhama. Tafadhali usisahau kutia saini na kujumuisha nambari yako **mpya** ya marejeo.

**MASWALI**
Ikiwa una maswali yoyote kuhusu maombi yako ya ulinzi wa kimataifa au barua hii, unapaswa kuwasiliana na **(taja nambari yako mpya ya marejeo**):

**Customer Service Centre**
**International Protection Office**
**Irish Naturalisation and Immigration Service**
**79 - 83 Lower Mount Street**
**Dublin 2, D02 ND99**
**Simu: 01 6028008**
**Barua pepe: info@ipo.gov.ie**

Ujumbe wa barua hii na viambatisho vinanakiliwa kwa mawakili wa kisheria.

**Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa**

**Huduma ya Uraia na Uhamiaji ya Ayalandi**

**Date**